



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

MAELEKEZO YA KISERA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi chini ya kifungu cha 3, 13(2) na 61(3)(a) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ikisomwa pamoja na kifungu cha 4 na cha 62(a) vya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, inatoa **MAELEKEZO YA KISERA KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020** kama ifuatavyo-


NA	CHANGAMOTO	MAELEKEZO
1.	Kutoonekana vizuri au kutokuonekana kabisa kwa picha ya mpiga kura (Kivuli) aliyejiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura ili hali taarifa zake nyingine zipo kwenye Daftari la kituo sawa na zile zilizoko kwenye Kadi ya Mpiga Kura.	Kwa mpiga kura ambaye picha yake haipo/haionekani katika Daftari la Wapiga Kura lakini ana kadi ya mpiga kura yenye taarifa binafsi sawa na zilizopo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, aruhusiwe kupiga kura.

NA	CHANGAMOTO	MAELEKEZO
2.	Kutofautiana kwa namba ya kadi ya mpiga kura na ile iliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wakati taarifa nyingine zote zikiwemo picha na taarifa binafsi zilizopo kwenye Daftari ni sawa na zilizopo katika kadi ya mpiga kura.	Kwa mpiga kura ambaye ana kadi yenye picha inayotofautiana na picha iliyo katika Daftari la Kudumu la Mpiga Kura aruhusiwe kupiga Kura.
3.	Wapiga kura ambao walijiandikisha na majina yao yapo kwenye Daftari la Wapiga Kura lakini kadi zao zimeharibika au kupotea.	Mpiga kura ambaye ameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini amepoteza Kadi yake ama kadi yake imeharibika na taarifa zake zipo katika Daftari aruhusiwe kupiga Kura kwa kutumia kitambulisho moja wapo kati ya vitambulisho vifuatavyo- i) Kitambulisho cha Utaifa (NIDA), ii) Leseni ya Udereva, au iii) Pasi ya kusafiria (Passport).
4.	Wapiga kura wenye kadi za kupigia kura lakini taarifa zao hazipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.	Wapiga kura ambao wana kadi ya kupigia kura lakini hawapo katika Daftari la Wapiga Kura, WASIRUHUSIWE KUPIGA KURA.

NA	CHANGAMOTO	MAELEKEZO
5.	<p>Mabadiliko ya mipaka ya kiutawala yaliyofanyika wakati au baada ya zoezi la uboreshaji kukamilika ambapo kuna mabadiliko ya jina la Kata ya Ilesa ambayo sasa inaitwa Buhunda na baadhi ya vijiji vya Kata hiyo viliamishwa Kata ya jirani ya Ilujamate.</p>	<p>Katika jimbo la Misungwi kulikuwa na mabadiliko ya jina la Kata ya Ilesa ambayo sasa inaitwa Buhunda na baadhi ya vijiji vya Kata hiyo kuhamishiwa Kata ya jirani ya Ilujamate wapiga kura wa kata hizo mbili watapiga kura kama ifuatavyo-</p> <ul style="list-style-type: none"> i) Wapiga kura wa vijiji vya Ilesa na Mbalama watapiga kura - katika Kata ya Ilujamate badala ya Kata ya Buhunda kupitia vituo walivyojiandikishia. ii) Wapiga kura wa kijiji cha Mwagimagi watapiga kura katika Kata ya Buhunda badala ya Kata ya Ilujamate kupitia vituo walivyojiandikishia. iii) Kituo cha SHULE YA MSINGI GUKWA kilichokuwa katika kijiji cha Nyang'homango Kata ya Ilujamate kimehamia katika kijiji kipyaa (Gukwa)

NA	CHANGAMOTO	MAELEKEZO
		kilichopo katika Kata ya Buhunda. Hivyo, Wapiga kura wa kituo hicho watapiga kura katika Kata ya Buhunda badala ya Kata ya Ilujamate.

Imetolewa na,


Dkt. Wilson Mahera Charles
MKURUGENZI WA UCHAGUZI
21 Oktoba, 2020